Mbiu ya
VIPIMO
TOLEO MAALUM LA MAADHIMISHO YA SIKU YA VIPIMO DUNIANI 2026
TOLEO NA. 006
JARIDA LA WAKALA WA VIPIMO (WMA)

# MAADHIMISHO YA SIKU YA VIPIMO DUNIANI YAFANA KITAIFA




*Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dennis Londo (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya viongozi wa Wizara na Taasisi zake, katika maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Vipimo Duniani, Mei 20 2026.*

HABARI UK. 3

# Maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani 2026: WMA Yatoa Taswira Mpya ya Kuthamini Watu, Kuelimisha Jamii na Kuwekeza kwa Vizazi Vijavyo

Kila mwaka tarehe 20 Mei, dunia huadhimisha Siku ya Vipimo Duniani kwa lengo la kuhamasisha umuhimu wa sayansi ya vipimo katika maendeleo ya uchumi, biashara, afya, viwanda na maisha ya kila siku. Kwa mwaka 2026, Wakala wa Vipimo (WMA) uliamua kuipa siku hiyo sura mpya kwa kuifanya isiwe tu siku ya kumbukizi ya kitaaluma, bali pia fursa ya kuifikia jamii, kuhamasisha kizazi kijacho na kuthamini wale walioweka msingi wa mafanikio ya taasisi.

Maadhimisho ya mwaka huu, yaliyobebwa na kaulimbiu "Sayansi ya Vipimo Isaidie Kujenga Imani katika Utungaji Sera," yalidhihirisha kuwa jukumu la Wakala wa Vipimo halipo tu katika kuhakiki mizani na vipimo, bali pia katika kujenga uelewa wa jamii kuhusu nafasi ya vipimo sahihi katika maendeleo ya Taifa.

Moja ya hatua zilizojitokeza kwa upekee ni uamuzi wa WMA kuwekeza kwa watoto na vijana kupitia kuanzisha Vilabu vya Vipimo (Vipimo Clubs) mashuleni. Huu ni uwekezaji wa muda mrefu na endelevu unaolenga kujenga kizazi kitakachokua kikielewa umuhimu wa vipimo sahihi katika maisha ya kila siku, biashara, sayansi na teknolojia. Elimu inayotolewa mapema huwajengea wanafunzi utamaduni wa kuthamini usahihi, uwajibikaji na haki, maadili ambayo ni msingi wa maendeleo endelevu ya Taifa.

Hatua nyingine iliyogusa wengi ni uamuzi wa WMA kuwakumbuka wastaafu wake katika maadhimisho hayo. Badala ya kuangalia mbele pekee, taasisi ilitazama pia nyuma kwa kutambua mchango wa wale walioijenga. Kuwaalika wastaafu kushiriki maadhimisho, kusikiliza historia zao, uzoefu wao, changamoto walizopitia na ushauri wao kwa watumishi wa sasa kulikuwa zaidi ya hafla ya kawaida; ilikuwa darasa la uongozi, utumishi na uzalendo.

Kitendo cha kuwakabidhi zawadi maalumu zenye kaulimbiu ya maadhimisho, pamoja na kuhakikisha hata wale ambao hawakuweza kufika wanafikishiwa zawadi zao kupitia ofisi za WMA katika mikoa mbalimbali, kilituma ujumbe muhimu kwamba mchango wa mtumishi hauishii siku ya kustaafu. Taasisi zinazothamini historia na watu wake hujenga utamaduni wa mshikamano, uaminifu na uwajibikaji.

Sambamba na hilo, WMA ilitumia maadhimisho hayo kupeleka elimu moja kwa moja kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini. Kupitia ukaguzi wa mizani katika masoko, vituo vya mafuta, hospitali, pamoja na maonesho na mikutano ya hadhara, wananchi walipata fursa ya kujifunza haki zao na namna ya kutambua vipimo sahihi. Elimu hiyo imeendelea kuwa nyenzo muhimu katika kupunguza udanganyifu wa kibiashara na kuongeza uelewa wa walaji na wafanyabiashara kuhusu wajibu wao wa kutumia vipimo vilivyohakikiwa.

Vyombo vya habari navyo vilikuwa mshirika muhimu katika maadhimisho hayo. Kupitia redio, televisheni, magazeti na majukwaa ya kidijitali, WMA iliweza kufikisha elimu ya vipimo kwa mamilioni ya Watanzania. Ushirikiano huu umeonesha kuwa jukumu la kulinda haki za mtumiaji haliwezi kutekelezwa na taasisi pekee, bali linahitaji ushiriki wa wadau mbalimbali, hususan vyombo vya habari vinavyofikisha taarifa kwa umma kwa wakati na kwa ufanisi.

Maadhimisho ya mwaka 2026 pia yamethibitisha kuwa elimu ni silaha muhimu katika kuimarisha matumizi ya vipimo sahihi. Mwananchi anayefahamu umuhimu wa mizani iliyohakikiwa, alama za uhakiki au madhara ya kutumia vipimo batili ana nafasi kubwa ya kudai haki yake na kushiriki katika kujenga mazingira ya biashara yenye uwazi na usawa.

Kwa kuunganisha elimu kwa jamii, uwekezaji kwa watoto na vijana, kuthamini wastaafu na kushirikiana na vyombo vya habari, WMA imeonesha mfano wa namna maadhimisho ya kitaifa yanavyoweza kutumika kuleta matokeo yenye manufaa ya kudumu badala ya kuwa shughuli za siku moja.


Kwa hakika, maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani 2026 yameacha alama muhimu ndani ya Wakala wa Vipimo na kwa jamii kwa ujumla. Yameonesha kuwa taasisi yenye mafanikio si ile inayotekeleza majukumu yake ya kisheria pekee, bali pia ile inayowekeza katika watu, inahifadhi historia yake, inajenga kizazi kijacho na inahakikisha elimu inawafikia wananchi wote.

Hiyo ndiyo taswira mpya ambayo Wakala wa Vipimo umeijenga kupitia maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani 2026 maadhimisho yaliyounganisha maarifa, historia, jamii na mustakabali wa Taifa. Kupitia hatua hizo, WMA imeendelea kuthibitisha kuwa usahihi wa vipimo si msingi wa biashara pekee, bali ni msingi wa uaminifu, maendeleo na ustawi wa jamii.

Mbiu ya VIPIMO
JARIDA LA WAKALA WA VIPIMO (WMA)

## BODI YA UHARIRI

| MWENYEKITI | MHARIRI MSAIDIZI |
|---|---|
| Alban Kihulla | Paulus Oluochi |
| **WAJUMBE** | **WAANDISHI** |
| Christopher Mwakibinga | Veronica Simba |
| Francis Olwelo | Paulus Oluochi |
| **MHARIRI MKUU** | **MSANIFU KURASA** |
| Veronica Simba | Lucas Gordon |



# MAADHIMISHO YA SIKU YA VIPIMO DUNIANI YAFANA KITAIFA



*Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dennis Londo (kulia), akisikiliza kwa umakini maelezo kutoka kwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA), Bw. Alban Kihulla, namna Wakala hiyo inavyohakiki dira za maji, ikiwa ni moja ya majukumu yake ya kila siku.*

**Dodoma**

Umuhimu wa vipimo sahihi katika kulinda haki za walaji na kuhakikisha uwepo wa biashara ya haki umeendelea kusisitizwa wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani yaliyofanyika kitaifa jijini Dodoma, Mei 20 2026 ambapo Wakala wa Vipimo (WMA) ulitumia jukwaa hilo kueleza kwa vitendo namna unavyotekeleza majukumu yake kwa manufaa ya wananchi na Taifa.

Maadhimisho hayo yaliratibiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara na kushirikisha baadhi ya taasisi zilizo chini ya wizara hiyo zinazohusika na usimamizi wa vipimo, huku yakilenga kuongeza uelewa wa jamii kuhusu mchango wa vipimo sahihi katika maendeleo ya uchumi, ulinzi wa walaji na kukuza biashara yenye ushindani wa haki.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Mgeni Rasmi, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dennis Londo, aliipongeza WMA kwa kazi kubwa ya kuhakiki na kuthibitisha usahihi wa vipimo vinavyotumika katika sekta mbalimbali nchini. Alisema kazi hiyo imeendelea kuimarisha uaminifu katika biashara na kuhakikisha wananchi wanapata bidhaa na huduma kulingana na kiasi wanachostahili.

"Wakala wa Vipimo mnafanya kazi muhimu ya kulinda haki za walaji na kuhakikisha biashara inafanyika kwa haki. Endeleeni kutekeleza majukumu yenu kwa weledi na uadilifu kwa maslahi ya Taifa na wananchi," alisema Mhe. Londo.

Katika maadhimisho hayo, Wakala wa Vipimo uliwasilisha mada kupitia video fupi iliyoonesha kwa kina majukumu yake ya msingi na namna yanavyotekelezwa katika kulinda maslahi ya wananchi. Video hiyo ilieleza kuwa Wakala unafanya ukaguzi, uhakiki na uthibitishaji wa usahihi wa mizani, pampu za mafuta, mita za maji, mita za umeme, mizani ya viwandani na vifaa vingine vya kupimia vinavyotumika katika shughuli za biashara nchini.

Kupitia ukaguzi huo wa mara kwa mara, Wakala huhakikisha kuwa vifaa vyote vya kupimia vinatoa matokeo sahihi ili kuzuia udanganyifu katika biashara. Hatua hiyo humwezesha mlaji kupata kiwango halisi cha bidhaa au huduma anayolipia, huku mfanyabiashara mwaminifu akipata mazingira ya ushindani wa haki.

Aidha, Wakala huendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutumia vipimo vilivyohakikiwa, namna ya kutambua alama za uhakiki na hatua zinazopaswa kuchukuliwa pale panapobainika matumizi ya vipimo visivyo sahihi. Elimu hiyo imekuwa nyenzo muhimu katika kuongeza uelewa wa wananchi na kuhamasisha ushiriki wao katika kulinda haki zao kama walaji.

Maadhimisho hayo pia yalihudhuriwa na wastaafu wa WMA pamoja na wanafunzi wa Shule ya Msingi Mtemi Mazengo kutoka jijini Dodoma, ambao ni wanachama wa VIPIMO Club. Kupitia klabu hiyo, wanafunzi hupata elimu kuhusu sayansi ya vipimo, matumizi yake katika maisha ya kila siku na umuhimu wa vipimo sahihi katika kujenga uchumi unaozingatia haki na uwazi.

Kuanzishwa kwa VIPIMO Club ni sehemu ya mkakati wa Wakala wa Vipimo wa kueneza elimu ya vipimo kwa wanafunzi katika shule mbalimbali nchini. Lengo ni kujenga kizazi chenye uelewa wa masuala ya vipimo tangu wakiwa wadogo, ili wawe mabalozi wa kuhamasisha matumizi ya vipimo sahihi katika familia zao na jamii kwa ujumla.

Ushiriki wa Wakala wa Vipimo katika Maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani umeonesha dhamira ya taasisi hiyo ya kuendelea kusimamia usahihi wa vipimo nchini, kulinda haki za walaji, kuimarisha uaminifu katika biashara na kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa kupitia mfumo wa vipimo unaozingatia viwango na sheria.




*Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA), Bw. Alban Kihulla (mwenye suti), na baadhi ya viongozi na watumishi wa WMA, wakiwa katika picha ya pamoja na wanachama wa Klabu ya Vipimo kutoka Shule ya Msingi Mtemi Mazengo iliyopo Dodoma, katika shamrashamra za maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Vipimo Duniani, Mei 20, 2026.*







*Matukio mbalimbali wakati wa maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Vipimo Duniani, Mei 20, 2026 jijini Dodoma.*

# HABARI KATIKA PICHA















*Matukio mbalimbali wakati wa maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Vipimo Duniani, Mei 20, 2026 jijini Dodoma.*

# HABARI KATIKA PICHA














*Matukio mbalimbali wakati wa maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Vipimo Duniani, Mei 20, 2026 jijini Dodoma.*

# HABARI KATIKA PICHA


















*Matukio mbalimbali wakati wa maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Vipimo Duniani, Mei 20, 2026 jijini Dodoma.*

# WAFANYABIASHARA DAR ES SALAAM WATAKIWA KUTUMIA VIPIMO SAHIHI

**Dar es Salaam**

Wafanyabiashara jijini Dar es Salaam wamehimizwa kuacha mara moja matumizi ya vipimo batili, ikiwemo kilicho maarufu kama 'lumbesa', na badala yake kutumia vipimo sahihi vilivyohakikiwa na Wakala wa Vipimo (WMA) ili kulinda haki za walaji na kujenga mazingira ya biashara yenye uadilifu na ushindani wa haki.

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Albert Chalamila, tarehe 18 Mei, 2026 katika Soko la Kariakoo wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kutokomeza matumizi ya vipimo batili, ikiwa ni sehemu ya maandalizi kuelekea Maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani yaliyofanyika kitaifa tarehe 20 Mei, 2026 jijini Dodoma.

Akizungumza na wafanyabiashara na viongozi wa masoko, Mhe. Chalamila alisema matumizi ya vipimo sahihi si suala la hiari bali ni takwa la kisheria na msingi muhimu wa kujenga uaminifu kati ya mfanyabiashara na mteja.

Alieleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inatambua mchango mkubwa wa wafanyabiashara katika kukuza uchumi wa Taifa, lakini mafanikio hayo hayapaswi kujengwa juu ya misingi ya udanganyifu.

"Serikali si adui wa wafanyabiashara. Tunathamini mchango wao katika kukuza uchumi wa Taifa. Hata hivyo, biashara lazima ifanyike kwa haki na uadilifu kwa kutumia vipimo sahihi," alisema Mhe. Chalamila.

Katika hotuba yake, Mkuu wa Mkoa aliwakumbusha wafanyabiashara kuwa wajibu wa kupima kwa usahihi umeelekezwa wazi katika vitabu vitakatifu vya Qur'an na Biblia, akisisitiza kuwa matumizi ya mizani na vifaa vya kupimia vilivyohakikiwa na Wakala wa Vipimo ni wajibu wa kisheria, si uchaguzi wa mfanyabiashara.

"Mwananchi anapokwenda sokoni kununua bidhaa anatarajia kupata kiasi sahihi cha bidhaa. Anapopata pungufu kwa sababu ya vipimo batili kama makopo, visado au lumbesa, tunapoteza uaminifu wake," alisisitiza.

Mhe. Chalamila aliwataka viongozi wa masoko kuwa walinzi wa kwanza wa matumizi ya vipimo sahihi kwa kuhakikisha vipimo batili havitumiki katika maeneo yao. Aidha, aliwahimiza wafanyabiashara kuwa mabalozi wa matumizi ya vipimo sahihi na kutoa taarifa wanapobaini vitendo vya udanganyifu vinavyohusisha matumizi ya vipimo visivyo halali.

Katika uzinduzi huo wa kampeni, Mkuu wa Mkoa alikabidhi tuzo iliyotolewa na Wakala wa Vipimo kwa viongozi wa Soko la Kisutu, baada ya kutambuliwa kuwa soko la mfano na kinara katika matumizi ya vipimo sahihi jijini Dar es Salaam.

Vilevile, aligawa mizani mikubwa yenye uwezo wa kupima hadi kilogramu 150 kwa viongozi wa masoko ya Ilala, Stereo Temeke, Machinga Complex, Mabibo na Kariakoo. Aidha, Soko la Kariakoo lilipokea mizani 20 ya kisasa ya kielektroniki yenye uwezo wa kilogramu 40, itakayogawiwa kwa wafanyabiashara ili kuboresha matumizi ya vipimo sahihi sokoni.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi wa Ufundi wa Wakala wa Vipimo, Bw. Francis Olwero, alimhakikishia Mkuu wa Mkoa kuwa Wakala utaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutumia vipimo sahihi katika biashara sambamba na kuimarisha ukaguzi wa kisheria na ukaguzi wa kushtukiza katika masoko mbalimbali nchini.

Alisema Wakala hautasita kuchukua hatua za kisheria dhidi ya mtu au mfanyabiashara yeyote atakayebainika kutumia vipimo visivyo sahihi au vinavyokiuka Sheria ya Vipimo.

Kampeni ya kutokomeza matumizi ya vipimo batili inalenga kuongeza uelewa wa wafanyabiashara na wananchi kuhusu umuhimu wa kutumia vipimo vilivyohakikiwa, kulinda haki za walaji na kuimarisha ushindani wa haki katika biashara.

Akihitimisha hotuba yake, Mhe. Chalamila aliwahimiza wananchi wa Jiji la Dar es Salaam kuendelea kujielimisha kuhusu haki yao ya msingi ya kupimiwa bidhaa kwa usahihi na kutoa taarifa kwa mamlaka husika wanapobaini matumizi ya vipimo batili.

Alisema ushirikiano kati ya Serikali, Wakala wa Vipimo, wafanyabiashara na wananchi ni nguzo muhimu katika kujenga mfumo wa biashara unaozingatia uwazi, haki na uaminifu, ambao ni msingi wa uchumi imara na endelevu.



*Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Albert Chalamila akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kutokomeza matumizi ya vipimo batili, Mei 18, 2026, Soko la Kariakoo jijini Dar es Salaam.*


Wakala wa vipimo
Tanzania
TOKOMEZA MATUMIZI
BATILI YA VIPIMO
#VipimoDay


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
WAKALA WA VIPIMO



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
WAKALA WA VIPIMO


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
WAKALA WA VIPIMO



# HABARI KATIKA PICHA

















# WMA KILIMANJARO YAADHIMISHA SIKU YA VIPIMO DUNIANI KWA KUTOA ELIMU SEKTA YA AFYA

**KILIMANJARO**

Katika kuadhimisha Siku ya Vipimo Duniani, Mei 20, 2026, Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Kilimanjaro uliendesha kampeni ya utoaji elimu kuhusu umuhimu wa matumizi sahihi ya vipimo katika sekta ya afya, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuhakikisha huduma za afya zinatolewa kwa kuzingatia usahihi wa vipimo.

Katika maadhimisho hayo, maafisa wa WMA walitembelea Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya St. Joseph, ambapo walitoa elimu kwa watumishi wa afya kuhusu umuhimu wa kutumia mizani iliyohakikiwa katika utoaji wa huduma za matibabu.

Mbali na utoaji wa elimu, Wakala ulifanya uhakiki wa mizani zinazotumika hospitalini hapo ili kujiridhisha kuwa zinatoa matokeo sahihi yanayoweza kutegemewa katika utoaji wa huduma kwa wagonjwa. Mizani zote zilizobainika kuwa na kasoro zilifanyiwa marekebisho na kurejeshwa katika hali ya kutoa vipimo sahihi.

WMA Kilimanjaro ilieleza kuwa matumizi ya mizani sahihi katika vituo vya kutolea huduma za afya ni muhimu kwa kuwa huchangia kufanya maamuzi sahihi ya kitabibu, ikiwemo kufuatilia maendeleo ya wagonjwa, kutoa dozi stahiki za dawa na kuhakikisha huduma za afya zinazingatia viwango vinavyotakiwa.

Uongozi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya St. Joseph ilipongeza Wakala wa Vipimo kwa kufikisha huduma hiyo hospitalini, ukisema imeongeza uelewa wa watumishi kuhusu umuhimu wa vipimo sahihi na kusaidia kuboresha ubora wa huduma zinazotolewa kwa wananchi.

Aidha, uongozi wa hospitali uliahidi kuendelea kushirikiana na Wakala wa Vipimo katika kuhakikisha vifaa vyote vinavyotumika kupima vinahakikiwa kwa wakati na vinaendelea kutoa matokeo sahihi kwa manufaa ya wagonjwa.

Maadhimisho hayo yameonyesha dhamira ya Wakala wa Vipimo ya kuendelea kusogeza huduma karibu na wananchi pamoja na kuongeza uelewa kuhusu nafasi ya sayansi ya vipimo katika kuboresha huduma za afya na kulinda usalama wa jamii.







*Watumishi wa Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Kilimanjaro wakitoa elimu kuhusu umuhimu wa matumizi sahihi ya vipimo katika sekta ya afya, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani, Mei 20, 2026.*

# WMA MWANZA WAADHIMISHA SIKU YA VIPIMO DUNIANI

**Mwanza**

Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Mwanza umeadhimisha Siku ya Vipimo Duniani kwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa matumizi ya vipimo sahihi katika biashara. Maadhimisho hayo yalifanyika katika Soko Kuu la Mwanza, yakilenga kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu haki yao ya kupata bidhaa zinazopimwa kwa usahihi.

Akizungumza wakati wa maadhimisho hayo, Meneja wa WMA Mkoa wa Mwanza, Karim Zuberi, alisema kuwa kila mwaka duniani huadhimishwa Siku ya Vipimo tarehe 20 Mei. Alieleza kuwa kaulimbiu ya mwaka huu ni "Vipimo Sahihi Hujenga Imani katika Utungaji wa Sera," ikisisitiza nafasi muhimu ya vipimo sahihi katika kuwezesha maamuzi na sera zinazotegemea takwimu sahihi.

Alifafanua kuwa mizani na vipimo sahihi vina mchango mkubwa katika upangaji wa bei, ujazo wa bidhaa na kulinda haki za walaji. Kwa sababu hiyo, WMA ilichagua kuadhimisha siku hiyo katika Soko Kuu la Mwanza kutokana na idadi kubwa ya wananchi wanaofanya shughuli za biashara na ununuzi wa bidhaa katika eneo hilo.

Bw. Zuberi alisema kuwa uhakiki wa mizani na vipimo ni jukumu endelevu la Wakala, linalotekelezwa mara kwa mara katika bucha, masoko, maduka, vituo vya mafuta, viwandani na kwenye bidhaa zinazoingizwa kutoka maeneo mbalimbali ili kuhakikisha wananchi wanapata bidhaa zenye uzito na ujazo sahihi.

Aidha, aliwataka wananchi kuhakikisha wanakagua mizani kabla ya kupimiwa bidhaa kwa kuangalia kama ina stika ya uhakiki ya WMA ya mwaka husika yenye nembo ya bibi na bwana, imebalansi vizuri na imewekwa sehemu inayoonekana wakati wa upimaji.

"Tutafuatilia uhakiki na upimaji mara kwa mara kwa kushtukiza katika maeneo yote yenye upimaji wa bidhaa," alisema Bw. Zuberi.

Pia aliwakumbusha wafanyabiashara kuacha kutumia sado, ndoo, makopo, mafungu na vifungashio visivyoidhinishwa katika kuuza bidhaa, kwani matumizi yake yanakiuka sheria za vipimo na yanaweza kusababisha walaji kupata bidhaa pungufu ya kiwango kinachostahili.

Kupitia maadhimisho hayo, Wakala wa Vipimo umeendelea kuhamasisha matumizi ya vipimo sahihi kama msingi wa biashara yenye haki, ulinzi wa mlaji na kuimarisha imani ya wananchi katika mifumo ya biashara nchini.







*Watumishi wa Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Mwanza wakiadhimisha Siku ya Vipimo Duniani (Mei 20, 2026) kwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa matumizi ya vipimo sahihi katika sekta ya biashara.*

# WMA PWANI YAKAGUA VITUO VYA MAFUTA IKIADHIMISHA SIKU YA VIPIMO DUNIANI

**PWANI**

Ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani, Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Pwani umeendesha zoezi la uhakiki wa mashine za mafuta katika vituo mbalimbali vya mafuta kwa lengo la kuhakikisha usahihi wa vipimo na kulinda haki za watumiaji.

Akizungumza wakati wa zoezi hilo, Meneja wa Wakala wa Vipimo Mkoa wa Pwani, Bw. Anderson Nelson, amesema ukaguzi huo ulilenga kuhakikisha wananchi wanapata kiwango halisi cha mafuta wanacholipia, huku ukiwa sehemu ya shughuli za kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa vipimo sahihi katika biashara.

Alisema baada ya mashine za mafuta kukaguliwa na kujiridhisha kuwa zinakidhi viwango vinavyotakiwa, Wakala huweka alama maalum inayoonesha kuwa mashine hiyo imehakikiwa rasmi.

"Baada ya kukagua, tunaweka alama zinazomwezesha mwananchi kutambua kama kipimo hicho kimehakikiwa au la," amesema Bw. Nelson.

Aidha, ameeleza kuwa Wakala huweka lakiri maalum kwenye mashine za mafuta ili kuzuia mtu yeyote kufanya mabadiliko yasiyo halali baada ya mashine kuhakikiwa.



*Baadhi ya Wafanyakazi wa Wakala wa Vipimo (WMA), Mkoa wa Pwani wakiwa katika picha ya pamoja muda mfupi kabla ya kuanza maadhimisho ya siku ya vipimo duniani, Mei 20, 2026.*

Kwa mujibu wake, lakiri hiyo hubeba nembo ya Wakala wa Vipimo pamoja na tarehe inayoonesha mwaka ambao mashine hiyo ilihakikiwa.

"Tukikuta lakiri imekatwa, imeharibiwa au haiko kama tulivyoiacha, tunachukua hatua za kisheria kwa kuwa tunaamini imeondolewa kwa makusudi ili kupunja wateja na kujipatia faida isiyo halali," alisisitiza.

Wakala wa Vipimo umehimiza wananchi kujenga utamaduni wa kuangalia alama za uhakiki na lakiri zilizowekwa kwenye mashine za mafuta kabla ya kujaza mafuta, ili kujiridhisha kuwa wanapata kiwango sahihi cha mafuta wanacholipia.

Baadhi ya madereva walioshuhudia zoezi hilo wameishukuru WMA kwa kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa vipimo sahihi, wakisema elimu hiyo imewawezesha kutambua namna ya kutofautisha mashine zilizohakikiwa na zile ambazo hazijathibitishwa.

Ukaguzi huo ambao hufanyika walau mara moja kila mwaka na nyakati nyingine kwa kushtukiza, umeendelea kuonesha dhamira ya Wakala wa Vipimo ya kuhakikisha biashara zote zinazotumia vipimo zinafanyika kwa uwazi, usahihi na haki, sambamba na kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu nafasi yao katika kulinda haki zao wanaponunua bidhaa na huduma.



*Kituo cha Mafuta*

# WMA KATAVI YAWAHIMIZA WAKULIMA KUTUMIA MIZANI, KUACHANA NA VIPIMO BATILI

**KATAVI**

Wakulima mkoani Katavi wamehimizwa kutumia mizani iliyohakikiwa katika mauzo ya mazao yao na kuachana na matumizi ya vipimo batili ili kujilinda dhidi ya hasara na kuhakikisha biashara inafanyika kwa haki kati ya muuzaji na mnunuzi.

Ushauri huo ulitolewa na Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Katavi, Bw. Mrinde Elihaki, wakati akizungumza katika kipindi cha 'Kumekucha Tanzania' kinachorushwa na Mpanda Radio FM, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani yaliyofanyika Mei 20, 2026.

Bw. Mrinde alisema matumizi ya mizani iliyohakikiwa ni njia pekee ya kuhakikisha wakulima wanapata thamani halisi ya mazao yao na kuondoa mianya ya udanganyifu inayotokana na matumizi ya vipimo visivyo rasmi.

"Mfanyabiashara anayekuja kununua mazao hawezi kukubali kutumia ndoo yako ya nyumbani, anakuja na ndoo yake. Kwa nini? Mara nyingi ndoo hiyo huwa imefanyiwa ujanja wa kuipanua ili iingize mazao mengi zaidi na kumpatia faida isiyo halali," alisema.

Aliongeza kuwa endapo biashara itaendelea kufanyika kwa kutumia ndoo na vipimo vingine visivyohakikiwa, baadhi ya wafanyabiashara watanunua kwa kipimo kikubwa na kuuza kwa kipimo kidogo, jambo linalowaumiza wakulima na kuwanyonya wanunuzi.

"Anaweza kununua kwa ndoo kubwa, lakini akifika kuuza anatumia ndoo nyingine ambayo ameiminya ili apate faida kubwa isiyo halali. Suluhisho ni kutumia mizani iliyohakikiwa," alisisitiza.

Katika maadhimisho hayo yenye kaulimbiu "Sayansi ya Vipimo Isaidie Kujenga Imani katika Utungaji Sera," wananchi wa Mkoa wa Katavi waliiomba WMA kuongeza juhudi za kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutumia vipimo sahihi katika shughuli za biashara.

Mmoja wa wananchi, Bi. Mary Julius Simba, alisema bado kuna uelewa mdogo kuhusu matumizi ya mizani, hususan kwa wakulima na wafanyabiashara wa mazao.

"Kwa mfano sisi wauza mahindi tumekuwa na changamoto sana ya vipimo. Unakuta mtu ametoka kijijini hajui kabisa umuhimu wa kutumia mizani. Akifika sokoni ukimweleza kuwa mahindi yanauzwa kwa mizani, anaona ni jambo geni kwa sababu hajawahi kupata elimu kuhusu matumizi ya vipimo sahihi," alisema.

Kwa mujibu wa Wakala wa Vipimo, utoaji wa elimu kwa umma ni sehemu ya mkakati wa kuimarisha matumizi ya vipimo sahihi nchini, kulinda haki za wakulima, wafanyabiashara na watumiaji, pamoja na kuhakikisha biashara zote zinafanyika kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Vipimo, Sura 340.

WMA imeeleza kuwa itaendelea kushirikiana na vyombo vya habari na wadau mbalimbali kutoa elimu kwa wananchi ili kujenga utamaduni wa kutumia mizani iliyohakikiwa na kuondoa kabisa matumizi ya vipimo batili katika biashara ya mazao nchini.




*Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Katavi, Bw. Mrinde Elihaki.*

# WMA DODOMA YAONYA BIASHARA ZA MAKADIRIO, YAHIMIZA MATUMIZI YA VIPIMO SAHIHI

**Dodoma**

Wakala wa Vipimo (WMA) umetoa onyo dhidi ya tabia ya kufanya biashara kwa makadirio, ukisema matumizi ya makopo, vifurushi na vipimo vingine visivyo rasmi huchangia hasara kwa wafanyabiashara na unyonyaji kwa wanunuzi, hali inayoweza kudhoofisha juhudi za kujenga uchumi imara.

Akizungumza jijini Dodoma Mei 19, 2026 kuelekea maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani yanayoadhimishwa kila mwaka Mei 20, Meneja wa Wakala wa Vipimo Mkoa wa Dodoma, Bw. Said Ibrahim, alisema WMA imeendelea kuendesha ukaguzi na uhakiki wa vipimo katika masoko, maduka na maghala ili kuhakikisha biashara zote zinafanyika kwa kuzingatia vipimo sahihi vilivyohakikiwa.

Alisema katika kuhamasisha matumizi ya vipimo sahihi, WMA ilikagua na kukabidhi mizani mitano kwa wafanyabiashara wa Soko Kuu la Majengo, ikiwa ni sehemu ya kampeni ya utoaji elimu kwa wafanyabiashara na wananchi kuhusu umuhimu wa kutumia vipimo vinavyotambuliwa kisheria.

"Haiwezekani kufikia uchumi imara ikiwa bado kuna watu wanaouza bidhaa kwa kutumia makopo au vifurushi badala ya mizani iliyohakikiwa rasmi na Serikali," alisema Bw. Said.

Aidha, alisisitiza kuwa WMA itaendelea kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika maeneo mbalimbali ya biashara ili kubaini wafanyabiashara wanaochezea mizani au kutumia vipimo visivyo sahihi, huku hatua za kisheria zikichukuliwa dhidi ya watakaobainika kukiuka sheria.

"Biashara inayofanyika kwa kukadiria inaweza kumsababishia mfanyabiashara hasara au kumnyonya mnunuzi. Ndiyo maana tunaendelea kutoa elimu na kuhamasisha matumizi sahihi ya mizani kwa wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla," alisema.

Kwa mujibu wa Bw. Said, maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani yanapaswa kuwa fursa ya kuwakumbusha wananchi umuhimu wa kutumia vipimo sahihi ili kulinda haki za pande zote mbili za biashara, muuzaji na mnunuzi, na kujenga mazingira ya biashara yenye uwazi, uaminifu na usawa.

Kwa upande wake, Makamu Mwenyekiti wa Soko Kuu la Majengo, Bw. Fred Grayson, aliishukuru WMA kwa kulichagua soko hilo kuwa sehemu ya kampeni ya kuhamasisha matumizi ya vipimo sahihi kuelekea maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani.







Naye mfanyabiashara wa soko hilo, Bi. Hadija Abdala, alisema matumizi ya mizani ni njia muhimu ya kumwepusha mfanyabiashara na hasara pamoja na kujenga imani kwa wateja. Aidha, aliwataka wanunuzi kudai kupimiwa bidhaa kwa kutumia mizani iliyohakikiwa kila wanapofanya manunuzi.

Kampeni hiyo ilikuwa ni sehemu ya maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani, iliyolenga kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu nafasi ya vipimo sahihi katika kulinda haki za watumiaji, kuimarisha ushindani wa haki katika biashara na kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa.

# WMA YAWAKUMBUKA WASTAAFU KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA VIPIMO DUNIANI 2026




*Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA) Bw. Alban Kihulla (katikati) akiwa katikati picha ya pamoja na baadhi ya wastaafu wa Wakala hiyo.*

**DODOMA**

Wakala wa Vipimo (WMA) umeadhimisha Siku ya Vipimo Duniani 2026 kwa namna ya kipekee kwa kuwakumbuka na kuwatambua wastaafu wake waliotoa mchango mkubwa katika maendeleo ya taasisi, ikiwa ni sehemu ya kuthamini kazi na huduma zao kwa Taifa.

Katika hafla iliyofanyika Makao Makuu ya WMA jijini Dodoma, wastaafu walikabidhiwa zawadi maalumu ya picha ya mbao yenye kaulimbiu ya maadhimisho ya mwaka 2026 isemayo, "Sayansi ya Vipimo Isaidie Kujenga Imani katika Utungaji Sera,"ikiwa ni ishara ya kutambua mchango wao katika kuimarisha sekta ya vipimo nchini.

Mbali na kukabidhiwa zawadi hizo, wastaafu walipata fursa ya kujumuika na watumishi wa sasa wa Wakala katika hafla fupi iliyoambatana na mazungumzo ya kubadilishana uzoefu. Katika hafla hiyo, walieleza historia zao tangu walipojiunga na Wakala wa Vipimo, safari ya utumishi wao, mafanikio waliyochangia kuyafikia, changamoto walizokutana nazo pamoja na mafunzo waliyojifunza katika kipindi chote cha utumishi wao.

Aidha, walitoa maoni na ushauri kuhusu mambo yanayoweza kuendelea kuimarisha utendaji wa Wakala, huku wakisisitiza umuhimu wa kuendelea kudumisha weledi, uadilifu na ubunifu katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi.

Watumishi wengi waliohudhuria hafla hiyo walieleza kuvutiwa na simulizi na ushuhuda wa wastaafu hao, wakisema umewasaidia kuifahamu historia ya Wakala wa Vipimo, kuelewa hatua ilikotoka na kuoanisha safari hiyo na mafanikio makubwa yaliyofikiwa hadi sasa.

Walieleza kuwa uzoefu huo umewajengea ari mpya ya kuendelea kuifanyia kazi taasisi kwa kujituma zaidi na kupongeza Uongozi wa WMA kwa kuanzisha utaratibu wa kuwaunganisha watumishi wa sasa na waliostaafu.

Kwa upande wao, wastaafu walishukuru Wakala wa Vipimo kwa kuwakumbuka na kuwapatia zawadi maalumu pamoja na kuwaalika kushiriki maadhimisho hayo. Walisema hatua hiyo imeonesha wazi kuwa mchango wao bado unathaminiwa hata baada ya kustaafu, jambo lililowapa faraja na kuwafanya wajisikie kuwa bado ni sehemu ya familia ya WMA.

"Hatukutarajia kuthaminiwa kwa namna hii. Kitendo cha kutukumbuka, kutualika na kutupatia zawadi kimetuonesha kuwa kazi tuliyoifanya imeendelea kuthaminiwa. Hili limetufariji na kutupa heshima kubwa," walieleza baadhi ya wastaafu.

Kwa wastaafu ambao hawakuweza kuhudhuria hafla hiyo jijini Dodoma, Wakala wa Vipimo ulihakikisha nao wanapata zawadi zao kwa kuziratibu zikabidhiwe katika maeneo wanayoishi kupitia Mameneja wa WMA wa mikoa husika. Hatua hiyo ililenga kuhakikisha hakuna mstaafu anayesahaulika katika kutambua mchango wake kwa maendeleo ya taasisi.

Kupitia maadhimisho hayo, Wakala wa Vipimo umeonesha kuwa pamoja na kuendelea kutekeleza jukumu lake la kusimamia usahihi wa vipimo nchini, unatambua pia umuhimu wa kuthamini watu waliochangia kujenga msingi wa mafanikio yake.

Tukio hilo limeimarisha mshikamano kati ya watumishi wa sasa na wastaafu na kuacha funzo muhimu la kuhifadhi historia ya taasisi, kuthamini mchango wa watangulizi na kujifunza kutoka kwenye uzoefu wao kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Wakala wa Vipimo.

# HABARI KATIKA PICHA




*Aliyekuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA) na Kamishna wa Vipimo, Bi. Stella Kahwa, akipokea zawadi hiyo nyumbani kwake jijini Dar es Salaam kutoka kwa Meneja wa WMA Mkoa wa Ilala, Bw. Muhono Nashon.*



*Aliyekuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA) na Kamishna wa Vipimo, Bi. Magdalena Chuwa, akipokea zawadi zawadi hiyo nyumbani kwake jijini Dar es Salaam kutoka kwa Meneja wa WMA Mkoa wa Temeke, Bw. Hilolimus Mahundi.*



# HABARI KATIKA PICHA



*Aliyekuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA) na Kamishna wa Vipimo, Dkt. Ludovic Manege akipokea zawadi hiyo nyumbani kwake jijini Dar es Salaam kutoka kwa Meneja wa WMA Mkoa wa Kinondoni, Bi. Lilian Mwombeki.*







# WMA YAIMARISHA HUDUMA ZA UHAKIKI WA VIPIMO, YAONGEZA MAPAMBANO DHIDI YA LUMBESA



*Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Judith Kapinga.*

**DODOMA**

Wakala wa Vipimo (WMA) umeendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi na kuongeza uwezo wa utoaji huduma kwa kununua vifaa vya kisasa vya uhakiki wa vipimo pamoja na kuanza mchakato wa ujenzi wa ofisi mpya katika mikoa ya Lindi na Songwe.

Hayo yalielezwa bungeni na Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Judith Kapinga, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Waziri Kapinga alisema hadi Aprili 2026, usanifu na michoro ya majengo ya ofisi hizo ulikuwa umekamilika, huku hatua inayofuata ikiwa ni kutangaza zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi.

Katika kuboresha utendaji kazi na huduma kwa wananchi, alisema WMA imenunua vifaa mbalimbali vya kisasa vya TEHAMA, ikiwemo kompyuta mpakato (laptop) 35, kompyuta za mezani (desktop) 28, scanner mbili, multifunction printer 20, mashine mbili za kunakili nyaraka (photocopier) pamoja na colour printer moja.

Aidha, alisema Wakala umekamilisha ununuzi wa vifaa 72 vya kitaalamu vinavyotumika katika ukaguzi na uhakiki wa vipimo mbalimbali ili kuongeza uwezo wa kitaalam wa watumishi na kupanua huduma za uhakiki nchini.

Vifaa hivyo ni pamoja na digital thermometer, CNG dispensing pump verifier, mizani za kielektroniki (electronic balances) 31, mass comparator mbili, flow meters nne, proving tanks 11, pressure gauges tisa, vifaa 40 vya ukaguzi wa vipimo kwa wakaguzi wa maeneo ya kazi (portable legal metrology test kits for field inspectors) pamoja na vifaa 20 vya kuhakiki mizani ya usahihi wa hali ya juu (legal metrology test kits for verifying high precision balances).

Kwa mujibu wa Waziri Kapinga, upatikanaji wa vifaa hivyo utaongeza wigo wa huduma za uhakiki wa vipimo katika maeneo mapya na kuwawezesha wananchi kupata huduma karibu zaidi.

Katika hatua nyingine, Waziri Kapinga alisema Serikali kupitia Wakala wa Vipimo inaendelea kukabiliana na changamoto ya matumizi ya lumbesa katika biashara ya mazao ya kilimo nchini.

Alisema Sheria ya Vipimo, Sura 340, inaelekeza kuwa mazao yanayofungashwa kwa uzito hayapaswi kuzidi kilogramu 100, pamoja na kiwango himilivu cha asilimia tano, huku ikisisitiza matumizi ya mizani iliyohakikiwa na Wakala wa Vipimo angalau mara moja kwa mwaka.

Alieleza kuwa katika kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara imeendesha operesheni tisa katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Pwani, Morogoro, Mbeya, Iringa na Njombe.

Kupitia operesheni hizo, magari 2,500 yaliyokuwa yakisafirisha mazao yalikaguliwa, ambapo magari 2,419 yalibainika kuzingatia matakwa ya sheria kwa kubeba mazao yaliyofungashwa kwa uzito usiozidi kilogramu 100.

Hata hivyo, magari 81 yalikutwa yamekiuka Sheria ya Vipimo, na hatua mbalimbali za kisheria zilichukuliwa dhidi ya wahusika, ikiwemo kutozwa faini za papo kwa papo na kuagizwa kufungasha upya mazao hayo kwa kuzingatia viwango vinavyotakiwa.

Waziri Kapinga alisema operesheni hizo zinaendelea kufanyika katika mikoa yote ya Tanzania Bara kupitia ofisi za WMA zilizopo nchini kote, kwa lengo la kutokomeza kabisa matumizi ya lumbesa na kuhakikisha biashara ya mazao inafanyika kwa kuzingatia sheria na vipimo sahihi.

Aidha, alisema Serikali imeendelea kusogeza huduma karibu na wananchi kwa kuanzisha vituo vya muda 5,050 katika kata, mitaa na vijiji kwa ajili ya utoaji wa huduma za uhakiki wa vipimo.

Pia alibainisha kuwa baadhi ya halmashauri za miji na wilaya, zikiwemo Mpanda, Kasulu na Kibondo, zimetunga sheria ndogo za ushuru wa mazao zinazosisitiza matumizi ya mizani iliyohakikiwa na Wakala wa Vipimo, hatua inayolenga kuimarisha biashara yenye uwazi, kulinda haki za wakulima na wafanyabiashara, pamoja na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

# SHABIBY AIPONGEZA WAKALA WA VIPIMO KWA KUIMARISHA USIMAMIZI WA VIPIMO NCHINI



*Mbunge wa Jimbo la Gairo, Mhe. Ahmed Shabiby akichangia mada bungeni.*

**DODOMA**

Mbunge wa Gairo, Mhe. Ahmed Shabiby, ameipongeza Wakala wa Vipimo (WMA) kwa kuendelea kutoa ushirikiano wa karibu kila inapohitajika katika kuhakikisha wananchi wanapata bidhaa na huduma zenye vipimo sahihi, hatua ambayo amesema imechangia kuimarisha usimamizi wa vipimo na kulinda maslahi ya wananchi pamoja na wafanyabiashara nchini.

Akichangia bungeni wakati wa mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Mhe. Shabiby alisema WMA imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi huku ikishirikiana kikamilifu na wadau mbalimbali katika kuhakikisha mfumo wa usimamizi wa vipimo nchini unaendelea kuimarika.

Katika mchango wake, Mhe. Shabiby alimpongeza Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo, Ndugu Alban Kihulla, kwa uongozi wake wenye weledi na ushirikiano mzuri katika kusimamia majukumu ya taasisi hiyo.

"Nimpongeze Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo kwa kazi nzuri na ushirikiano ambao wamekuwa wakitoa kila wanapohitajika. Wameendelea kusimamia vyema masuala ya vipimo kwa manufaa ya wananchi," alisema Mhe. Shabiby.

Pamoja na pongezi hizo, Mbunge huyo aliitaka WMA kuongeza umakini katika kusimamia usahihi wa vipimo vya bidhaa za chuma, hususan nondo zinazozalishwa na baadhi ya viwanda nchini, akisema bado kuna changamoto ya bidhaa hizo kutokidhi viwango vinavyotakiwa.

Ameeleza kuwa baadhi ya viwanda vinavyoendeshwa na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi vinaendelea kuzalisha nondo zisizo na vipimo sahihi, hali ambayo inaweza kuhatarisha usalama wa majengo na maisha ya wananchi.

"Tusibaki kwenye kutoa faini pekee. Viwanda vinavyotengeneza nondo zisizokidhi vipimo vinapaswa kuchukuliwa hatua kali, ikiwemo kufungiwa, ili kulinda usalama wa wananchi na ubora wa ujenzi nchini," alisema Mhe. Shabiby.

Aidha, alisisitiza kuwa usimamizi madhubuti wa vipimo vya bidhaa za ujenzi ni msingi muhimu wa kukuza sekta ya viwanda, kuimarisha ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini na kulinda usalama wa miundombinu.

Kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo, Sura 340, Wakala wa Vipimo una jukumu la kusimamia matumizi sahihi ya vipimo nchini ili kuhakikisha wananchi wanapata bidhaa na huduma zinazolingana na thamani ya fedha wanazolipa, sambamba na kujenga mazingira ya biashara yenye haki na ushindani wa usawa.

# WMA YAWAPONGEZA WATUMISHI WAKE MEI MOSI

**NJOMBE**

Wakala wa Vipimo (WMA) umewapongeza watumishi wake kwa mchango wao mkubwa katika kulinda haki za watumiaji na kujenga uchumi imara kupitia usimamizi wa matumizi ya vipimo sahihi vinavyokidhi viwango vinavyokubalika kimataifa.

Pongezi hizo zimetolewa na Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo, Ndugu Alban Kihulla, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) yaliyofanyika mkoani Njombe.

Akizungumza na watumishi wa Wakala, Kihulla amesema anajivunia kiwango cha kujituma, uadilifu na weledi wanaouonesha kila siku katika kutekeleza majukumu ya uhakiki na ukaguzi wa vipimo pamoja na ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa.

"Ninajivunia kujituma kwenu, uadilifu na weledi mnaouonesha kila siku katika uhakiki na ukaguzi wa vipimo pamoja na ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa. Kazi yenu ina mchango mkubwa katika kuimarisha biashara yenye haki, kuongeza imani kwa walaji na kukuza maendeleo ya Taifa letu," amesema Kihulla.

Amesema katika kipindi hiki cha maendeleo ya teknolojia na ukuaji wa sekta mbalimbali za uchumi, watumishi wa WMA wameendelea kujifunza, kuongeza ujuzi na kuboresha utendaji wao ili kuendana na mahitaji mapya ya kazi na matarajio ya wananchi.

Aidha, amewahimiza watumishi kuendelea kushikamana, kudumisha nidhamu ya kazi na kuzingatia maadili ya utumishi wa umma ili Wakala uendelee kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Endeleeni kushikamana, kudumisha nidhamu ya kazi na kuzingatia maadili ya utumishi wa umma. Uongozi wa Wakala unatambua na kuthamini mchango wenu na utaendelea kuboresha mazingira ya kazi ili muweze kutekeleza majukumu yenu kwa ufanisi zaidi," amesema.


Kihulla amesisitiza kuwa Wakala wa Vipimo utaendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ili kuhakikisha wananchi wanapata bidhaa na huduma zenye vipimo sahihi, huku ukidhibiti vitendo vya udanganyifu vinavyofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu.

Ameongeza kuwa watumishi wa WMA katika mikoa yote nchini wataendelea kuendesha operesheni za mara kwa mara za ukaguzi na utekelezaji wa sheria ili kuwabaini na kuwachukulia hatua wanaojihusisha na vitendo vya kuhujumu mfumo wa vipimo, wakiwemo wanaotumia **lumbesa** na mbinu nyingine za kuwapunja wakulima, wafanyabiashara na watumiaji.

Amesema mafanikio ya Wakala yanategemea ari, uadilifu na mshikamano wa watumishi wake, huku akisisitiza kuwa WMA itaendelea kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha biashara nchini inafanyika kwa kuzingatia vipimo sahihi, haki na viwango vinavyolinda maslahi ya wananchi na kuchochea maendeleo ya uchumi wa Taifa.



*Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo (WMA) Bw. Alban Kihulla.*



WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA

WAKALA WA VIPIMO

Ndugu Watumishi wa Wakala wa Vipimo.

Mshikamano Solidarity

Naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati katika kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi). Hii ni siku muhimu ya kutambua mchango wenu mkubwa katika kujenga uchumi imara kupitia matumizi sahihi ya Vipimo vilivyo katika usahihi unaokubalika kimataifa.

Ninajivunia kujituma kwenu, uadilifu, na weledi mnaouonesha kila siku katika uhakiki na ukaguzi wa Vipimo pamoja na ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa.
Kazi yenu ina mchango mkubwa katika kuimarisha biashara yenye haki, kuongeza imani kwa walaji, na kukuza maendeleo ya taifa letu.

Katika kipindi hiki cha mabadiliko ya teknolojia na ukuaji wa sekta mbalimbali, nawapongeza kwa kuendelea kujifunza, kuboresha ufanisi, na kuendana na mahitaji mapya ya kazi. Endeleeni kushikamana, kudumisha nidhamu ya kazi, na kuzingatia maadili ya utumishi wa umma.


Uongozi wa Wakala unatambua na kuthamini mchango wenu, na utaendelea kuboresha mazingira ya kazi ili muweze kutekeleza majukumu yenu kwa ufanisi zaidi.

Hongereni sana kwa kazi nzuri, na heri ya Mei Mosi

Mbiu ya

# VIPIMO

JARIDA LA WAKALA WA VIPIMO




## MAWASILIANO:

Wakala wa Vipimo (WMA)
7 Mtaa wa Mkemia Mkuu, S.L.P 2014
41104 Tambukareli, Dodoma.

wakalawavipimotanzania | Piga Bure 0800110097 | www.wma.go.tz